

HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI



KOTESHENI NA.LGA/024/2017-2018/W/23 LOT V - VIII

KWA AJILI YA KUPATA MAFUNDI WA KUJENGA MAJENGU YA KUTOLEA HUDUMA
KATIKA KITUO CHA AFYA MUNDEMU

MWALIKO WA KOTESHENI

TAREHE: 27/02/2018


1. Halmashauri ya Wilaya ya Bahi imepokea fedha kutoka HAZINA kwa ajili ya kujenga Miundombinu katika Kituo cha Afya Mundemu kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo itatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao utatolewa katika huu Mwaliko wa Kotesheni.
2. Unakaribishwa kuomba kwa barua Kotesheni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye jedwali la Mchanganuo hapo chini kwa ajili ya kujaza bei yako katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri siku za kazi kuanzia tarehe 28/02/2018.

NA	KOTESHENI NAMBA	LOT NA:	MAELEZO YA KAZI
1	KOTESHENI NA.LGA/024/2017-2018/W/23	V	Ujenzi wa Kichomea taka
		VI	Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti na shimo la kutupa kondo la nyuma
		VII	Ujenzi wa njia za kutembelea (walkways)
		VIII	Ujenzi wa tenki la kuvunia maji ya mvua, mnara wa kuwekea tenki la maji na chumba cha kuhifadhia mitambo ya kuzalisha oksijeni

*Mwombaji anaweza kuomba kazi zaidi ya moja

3. Kotesheni kwa ajili ya kujaza bei itapatikana ofisi ya Manunuzi, Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi baada ya kulipa ada ya maombi ya **shilingi elfu thelathini (Tsh.30,000.00/=)** ambayo haitarejeshwa [Non-refundable] na Malipo yatafanyika katika ofisi ya Mweka Hazina (W) Bahi kuanzia saa **1.30 asubuhi** hadi saa **9.30 alasiri**.

4. Sifa za Mwombaji;
 - Bei ya zabuni iliyojazwa kikamilifu na kutiwa saini kulingana na Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (sehemu ya 2 katika kotesheni).
 - Orodha ya mikataba iliyofanywa hivi karibuni inayofanana na hii pamoja na majina na anwani za Waajiri kwa ajili ya kuthibitisha.
 - Awe na elimu ya ufundi ujenzi kwa kiwango chochote aambatanishe nakala za vyeti vya mafunzo.
 - Awe hajawahi kutokamilisha mradi wowote wa ujenzi ndani na nje ya Halmashauri.
 - Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani za majengo.
5. Kila mwombaji anatakiwa kurejesha Kotesheni katika uhalisia wake (original) moja iliyojazwa kwa usahihi na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "**Kotesheni Na. LGA/024/2017/2018/W/23 Lot Na.... Na maelezo ya kazi husika.** Ni lazima zipelekwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, Ofisi ya Manunuzi, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, S.L.P 2993, Dodoma.
6. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni tarehe **06/03/2018** kabla au ifikiapo saa **7:00 mchana**. Kotesheni hizo zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa waombaji wanaoamua kuhuduria katika ufunguzi wa kotesheni katika Ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.
7. Kotesheni zitakazochelewa na zisizofunguliwa katika kikao cha ufunguzi wa kotesheni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa hali yoyote ile.



Rachel M. Chuwa
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BAHI